

UNIVERSITY OF CAMBRIDGE INTERNATIONAL EXAMINATIONS
General Certificate of Education Ordinary Level

SWAHILI

3162/01

May/June 2005

2 hours 30 minutes

Additional Materials: Answer Booklet/Paper

READ THESE INSTRUCTIONS FIRST

If you have been given an Answer Booklet, follow the instructions on the front cover of the Booklet.
Write your Centre number, candidate number and name on all the work you hand in.
Write in dark blue or black pen on both sides of the paper.
Do not use staples, paper clips, highlighters, glue or correction fluid.

Answer **all** questions.

At the end of the examination, fasten all your work securely together.

The number of marks is given in brackets [] at the end of each question or part question.

1 Translate into **English**:

- (a) Usafi ni kitu muhimu katika maisha ya watu wa miji mikubwa kama vile Dar es Salaam na Nairobi. Hakuna mtu anayeishi mjini asiyetaka mji wake uwe safi. Nina hakika kwamba mji safi ni lengo la kila mwananchi. Basi, je, lengo hili litatekeleka vipi? Baraza la Manispaa limependekeza njia mbili zinazohitajiwa kufuatwa na wananchi. Kusema kweli, njia zenyewe si ngumu hata kidogo. Njia ya kwanza inamtaka kila mtu kutotupa taka ovyo. Taka zitupwe kwenye sehemu zilizotengwa kwa ajili hiyo. Wenye nyumba waliopewa mapipa ya taka lazima wazitie taka humo. Tena wasifanye uvivu wa kuyaweka mapipa nje ya nyumba zao ili matopasi waweze kuzichukua taka.

Njia ya pili ni kuwaelimisha wananchi juu ya hatari zinazotokana na taka. Taka zinazotupwa ovyo zinaweza kuleta maradhi. Kwa mfano, baadhi ya watu wana tabia mbaya ya kutupa makombo ya vyakula nje ya nyumba. Taka kama hizi huoza na kutoa mafunza. Wazee wanahimizwa wawafunze watoto wao usafi nyumbani. [20]

- (b) Ugonjwa wa UKIMWI umeleta madhara ya aina nyingi duniani kwa jamaa za wale wagonjwa waliofariki. Ni jambo la kusikitisha kwamba hivi leo kuna idadi kubwa ya watoto yatima Afrika ya Mashariki ambao baba na mama zao wamefariki kutokana na ugonjwa hatari huu. Watoto hawa mara nyingi hutazamwa na jamaa wa akina mama na baba. Lakini ikiwa jamaa wenyewe ni masikini, au wana femelia kubwa, inakuwa vigumu kwao kutekeleza mahitaji ya watoto yatima hawa. Hapo serikali na mashirika huwasaidia kadiri yawezavyo.

Misaada inayotolewa na mashirika huwasaidia watoto yatima hawa kwa njia tatu – kuwatafutia mahala pa kukaa, kuwapatia chakula na nguo, na kuwanunulia sare za shule, madaftari, kalamu, viatu na kuwalipia ada za shule. Kwa vile idadi ya watoto yatima ni kubwa, sio wote wanaopata msaada. Mashirika sasa yanazingatia wazo la kuungana mikono ili wafanye kazi pamoja. Kwa kuchanganya misaada yao, wataweza kuwasaidia watoto wengi zaidi kuliko wafanyavyo sasa. [25]

2 Translate into Swahili:

It is not unusual nowadays to hear parents complain about the conduct and habits of youths. They say that the youths of today behave more improperly than did those of the past. According to their parents, this can be seen in three areas. Firstly, the youths today show less respect for the elders. They do not stand up to greet an elder when he enters a room; they do not offer a seat to him; and they sit disrespectfully with their legs crossed as if they were in a bar. Secondly, their language lacks respect. They do not seem able to hold a conversation without using swearwords. As a result, younger children then use such words in their conversation sometimes without understanding their meaning. And finally, the clothes youths wear also show disrespect. Many elders in African societies do not like girls to wear jeans or short skirts.

Although I am no longer a youth – my age is now approaching 50 years – I want to defend our youths. Parents seem to forget that such complaints occur in every generation, because each generation lives by the style of its time. [30]

3 Write about 120 words in Swahili on one of the following subjects:

- (a) The importance of the seas and oceans.
- (b) Do you think that mobile phones are useful? Give reasons for your answer.
- (c) In your local newspaper, it was reported that some people in your town are very cruel to animals. Write a letter to the editor suggesting ways of stopping the cruelty. [25]

